MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.28: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya July 1-10, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Julai 11-20, 2026*

## MUHTASARI

- Mvua nyepesi zinazotarajiwa katika maeneo machache husuan Pwani ya kaskazini na kanda ya Ziwa Victoria zinaweza kusaidia kuongezeka kwa unyevunyevu katika udongo na kusaidia upatikanaji wa malisho kwa ajili ya wanyama. Pia hali hii inaweza kuathiri shughuli za ukaushaji na uhifadhi wa mazao.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itasaidia katika shuguli za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao ghalani.
- Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu kutoka mashariki kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani uliimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Katika dikadi hii, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu isipokuwa katika maeneo machache ya ukanda wa Pwani na mikoa ya Kilimanjaro na Mara, ambayo yalipata mvua ya siku kumi ya kiasi cha milimita 1 hadi 25. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya Mara na Dar es Salaam yalipata mvua kati ya milimita 26 hadi 100 kama inavyooneshwa katika Kielelezo.




*Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha July 1-10, 2026*

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Katika dikadi hii, hali ya ukavu inayoendelea katika maeneo mengi nchini ilisaidia uvunaji, ukaushaji na kuhifadhi mazao maghalani hususan mahindi na mpunga. Hata hivyo, hali ya mvua iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo nchini husuan Pwani ya kaskazini na kanda ya Ziwa Victoria ilisaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao ya nje ya msimu ikiwemo maharagwe katika wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Zao la alizeti liko katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Dodoma, Morogro na Singida.

Kwa upande wa mazao ya kudumu, zao la kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe ilikuwa katika hatua ya vitunda vigumu “***berry hard***”.

Kwa upande mwingine, karafuu katika Visiwa vya Pemba na wilya ya Mheza mkoani Tanga, zilikuwa katika hatua ya karafuu changa na kuanza kukomaa.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori umeanza kupungua kutokana na hali ya ukavu iliyopo.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kimeendelea kupungua kidogo kutokanana na hali ya ukavu inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2026

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa Dunia inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kudumisha mwenendo wa ukandamvua kuelekea kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu.
Aidha, kuimarika kwa mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani vinatarajiwa kuendelea kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2026

Maeneo kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), yanatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi), Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kupata vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Maeneo ya nyanda za juu kusini-magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) pamoja na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2026

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayotarajiwa kupata hali hiyo, itasaidia katika shughui za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao maghalani. Hata hivyo, hali ya mvua nyepesi inayotarajiwa katika maeneo machache inaweza kusaidia kuongeza unyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa majani ya malisho kwa ajili ya wanyama. Pia hali hii inaweza kuathiri shughuli za ukaushaji na uhifadhi wa mazao.

**USHAURI**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu za kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini):** Wakulima wanashauriwa kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku na kujiandaa na mvua za muda mfupi zinazotarajiwa katika maeneo machache.

- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (pwani ya kusini, maeneo ya magharibi, maeneo ya kati, nyanda za juu za kusini magharibi na maeneo ya kusini):** Wakulima wanashauriwa kuendelea kuvuna mazao na kuyahifadhi vizuri maghalani huku wakiendelea kufuatili tarifa za hali ya hewa za kila siku.

- **Kwa maeneo yote:** Wafugaji wanashauriwa kuendelea kutunza mifugo yao na kuvuna maji ya mvua kila iwezekavyo kwa ajili ya matumizi ya baadae.

- **Wavuvi wanaotumia Bahari kuu na Maziwa makubwa:** Wanashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku ili kuchukua tahadhari hususan wakati vinapojitokeza vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa majini. Pia wanashauriwa kukaa karibu na bandari salama wakati wa mvua za radi zinazotarajiwa katika maeneo machache hususan katika kanda ya ziwa Victoria.

Ushauri huu unalenga kuongeza tija ya kilimo na kupunguza athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kutumia taarifa za hali ya hewa kwa ufanisi na kushauriana na maafisa kilimo katika maeneo yao ili kufanya kilimo chenye tija.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kupungua kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Jamii inashauriwa kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Mkurugenzi Mkuu
S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)